# Ajali yakatisha uhai bodaboda, abiria, waenda kwa miguu

Na Hamisi Nasri, *MASASI*
0715086344 WhatsApp / SMS

WATU wanne, wakazi wa Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, wamefariki dunia papo hapo kutokana na ajali ya barabarani iliyohusisha gari moja kugonga pikipiki na baadaye kuwagonga watembea kwa miguu waliokuwa pembeni mwa barabara.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Kamishina Msaidizi wa Polisi (ACP) Mtaki Kurwijila, ajali hiyo ilitokea Mei 23 majira ya saa nne usiku katika eneo la barabara ya Rest Camp kuelekea Tunduru.

ACP Kurwijila alisema ajali hiyo ilihusisha gari lenye namba za usajili DFP 3064 aina ya Toyota Land Cruiser ambalo dereva wake hajafahamika.

> **Dereva alishindwa kulimudu gari lake na kuhama upande wa kushoto wa barabara, kisha kugonga pikipiki na baadaye watembea kwa miguu,**

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, gari hilo lilihama upande wa kushoto wa barabara na kisha kwenda upande wa kulia, ambako liligongana uso kwa uso na pikipiki yenye namba MC 984 DUX aina ya TVS.

Pikipiki hiyo ilikuwa ikiendeshwa na Stuwart Daniel (21), akiwa na abiria Noel Dastan (21), wote wakazi wa mtaa wa Nangaya, Masasi. Wote wawili walifariki dunia papo hapo kutokana na ukubwa wa ajali hiyo.

Baada ya hapo, gari hilo lilipoteza mwelekeo na kuwagonga watembea kwa miguu wawili waliokuwa pembeni ya barabara, ambao majina yao hayajafahamika, na nao pia walifariki dunia papo hapo.

Kaimu Kamanda huyo wa Polisi alisema miili ya marehemu wote wanne imehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti cha Hospitali ya Mkomaindo, Masasi, huku taratibu za kuwatambua na kuwasiliana na ndugu zao zikiendelea.

Aliongeza kuwa dereva wa gari hilo alikimbia baada ya ajali na anatafutwa na Jeshi la Polisi kwa ajili ya hatua za kisheria.

Kwa mujibu wa Jeshi la Polisi, chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva pamoja na mwendo kasi uliosababisha kushindwa kulimudu gari na hatimaye kuhama njia.

"Dereva alishindwa kulimudu gari lake na kuhama upande wa kushoto wa barabara, kisha kugonga pikipiki na baadaye watembea kwa miguu," ACP